# Kwa Wazazi na Walezi: Haki na Mambo yenye inakupasa ku fanya ku Masomo ya Mtoto Wako

Watoto na vijana wote mu inchi ya Marekani wako na haki ya kupata elimu kwa bure mu masomo ya serikali, bila kujali hali yao ya uhamiaji, luga, ao kiwango yao ya masomo.



## Haki za Wazazi na Walezi:



Kupata habari kutoka ku masomo mu luga yenye unaelewa. Hizi huduma za tafsiri zinapashwa tolewa kwa bure na zinapashwa tolewa na batu benye bako na ujuzi ya kufanya ile kazi.



Kujua maendeleo ya mtoto wako ku masomo na kulomba kukutanana na walimu wakati yoyote mu mwaka wa masomo.



Kulomba msaada ku masomo kama mtoto wako iko na shida ya kujifunza, shida ya afya ao tabia zenye zinazuwiya uwezo wake wa kujifunza.



Kupokea habari kutoka ku masomo kuhusu mwenendo na shuguli za mtoto wako.

## Mambo yenye inapasa Wazazi na Walezi kufanya:

- [ ] Hakikisha mtoto wako anaenda ku masomo kila siku, na ujulishe masomo kama atakosa
- [ ] Jibiya maswali kutoka kwa bafanyakazi ba ku masomo na ubaendeye saa uko na wasiwasi kuhusu masomo, tabia ao unyanyasaji wa mtoto wako.
- [ ] Tengeneza mazingira tulivu ya kujifunzia kunyumba, himiza tabia za muzuri za kujifunza, na uhakikishe kazi za masomo za kufanyiya kunyumba zinamalizika.
- [ ] Hakikisha mtoto wako anasinziya ya kutosha, anakula muzuri na anajisikiya anaungwa mukono.
- [ ] Mufundishe mtoto wako umuhimu wa heshima, wajibu na kushiriki kikamilifu mu shuguli za masomo.
- [ ] Endelea kukuwa na habiri kuhusu kuenda ya mtoto wako ku masomo, halama zake ku masomo na vifaa yenye inapatikana.
- [ ] Huzuria mikutano na shuguli za masomo, na ujitolee kusaidia wakati inawezekana.